Tangazo La Serikali Na. 659 La Tarehe 8/9/2023

SHERIA YA USIMAMIZI WA USHURU WA BIDHAA,
(SURA YA 147)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 128)*

AMRI YA MSAMAHA WA KODI KWA GARI MOJA LINALOINGIZWA NCHINI LA MRADI WA UANZISHAJI WA KITUO CHA UBUNIFU NA MAFUNZO YA UPIMAJI NA RAMANI WA WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI YA MWAKA 2023

Jina na kuanza kutumika

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Kodi kwa Gari Moja linaloingizwa nchini la Mradi wa Uanzishaji wa Kituo cha Ubunifu na Mafunzo ya Upimaji na Ramani wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ya Mwaka 2023, na itachukuliwa kuwa ilianza kutumika kuanzia tarehe 25 Julai, 2023.

Msamaha

2. Kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika aya ya 3, na masharti mengine yoyote yanayoweza kuimarishwa na Kamishna, kiasi chote cha kodi kinachotakiwa kulipwa kuhusiana na gari moja iliyoainishwa kwenye Jedwali, linavyoingizwa au kununuliwa ndani ya nchi, kabla ya kibali cha forodha na kwa niaba ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa ajili ya kutumika mahususi katika utekelezaji wa mradi wa kituo cha Ubunifu na Mafunzo ya Upimaji na Ramani nchini kimesamehewa.

Masharti

3. Msamaha wa kodi unaotolewa chini ya Amri hii utafikia ukomo na ushuru utadaiwa na utatakiwa kulipwa kana kwamba Amri hii haikutolewa, iwapo gari husika litatumika kwa madhumuni tofauti au litahamishwa,

kuuzwa au kwa namna yoyote kupewa mtu mwingine asiyestahili kufaidika na faida zinazotolewa chini ya Amri hii.

Kuisha kwa muda

4. Msamaha uliotolewa chini ya Amri hii utafikia ukomo tarehe 25 Januari, 2024.

**JEDWALI**

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

| Na. | Maelezo | Namba ya Chesesi | Namba ya Injini |
|---|---|---|---|
| 1. | Nissan X-Trial 2.0L Petrol 4WD 7-Seater SUV Model | JN1JANT32Z0013162 | MR20008684D |

Dodoma,
25th August, 2023.

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU
*Waziri wa Fedha*